

Jina la Sera	Sera ya Malipo ya Bajeti - Kitengo cha Usimamizi wa Mapato	Kitambulisho cha Sera	17373
Maneno muhimu	Bajeti, Kulipa, Malipo, Mpango, Wakati, RMD (Revenue Management Division – Idara ya Usimamizi wa Mapato), Mapato, Usimamizi		

I. Kusudi la Sera

Kusanifisha mchakato wa kuunda na kudumisha mpango wa bajeti ya malipo.

II. Wigo wa Sera

Utaratibu huu unahusu vituo vyote vya Dartmouth Health vilivyo kwenye mfumo wa biashara wa eDH (eDH business system).

III. Ufafanuzi

Madai ya deni: Wakati akaunti inakaa kwenye mfumo kwa muda mrefu kwa sababu ya kutolipwa kwa deni.

Dartmouth Health: Kwa makusudi ya sera hii, Wanachama wa Mfumo wa Dartmouth Health (DH) ni Alice Peck Day Memorial Hospital, Cheshire Medical Center, Dartmouth Hitchcock Clinic, Mt. Ascutney Hospital and Health Center, New London Hospital, Mary Hitchcock Memorial Hospital, Southern Vermont Medical Center (SVMC), Valley Regional Hospital, na Visiting Nurse and Hospice for Vermont na New Hampshire (VNH). Hospitali nyingine zote zinazopatikana New Hampshire na Vermont zinazingatiwa kuwa Si vituo Wanachama.

Sera hii inatumika kwa vituo wanachama wa DH vinavyotumia mfumo wa Epic.

IV. Taarifa ya Sera

- Mipango ya bajeti huundwa ndani ya kikomo cha kipindi cha miezi 36; tumia jedwali lifuatalo ili kufafanua istilahi za mpango.

Deni Lililosalia	Muda wa Malipo Uliopendekezwa	Upeo wa juu wa Muda wa Malipo
Chini ya \$1000.00	Miezi 12	Miezi 18
\$1001.00 hadi \$5000.00	-	Miezi 24
Zaidi ya \$5000.00	-	Miezi 36

- Kwa wagonjwa wanaoishi Vermont na ambao wanastahiki Usaidizi wa Kifedha (Financial Assistance), malipo ya mpango wa bajeti (budget plan payments) hayawezi kuhitaji malipo yanayozidi 5% ya jumla ya mapato ya kaya kwa mwezi.

- Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja (Customer Service Director) au Mkurugenzi wa Ustahiki na Usajili (Director of Eligibility and Enrollment) anaweza kuidhinisha kuongeza muda wa masharti yaliyoelezwa hapo juu kwa 20% inapohitajika.
- Hali maalum za ziada zinapaswa kuelekezwa kwa Mkurugenzi wa Usimamizi wa Mapato.
- Masalio mapya yanaongezwa kwa ombi la mgonjwa kupitia kupiga namba ya simu ya Huduma kwa Wateja, au kwa wao kuingiza akaunti kupitia myDH, ambayo itapanga upya kiasi kinachotakiwa kulipwa kwa bajeti na kuweka upya akaunti hizo katika kiwango cha malipo binafsi (self-pay level 1) na kuzuia akaunti hiyo kutoka kwenye utaratibu wa kudai deni.

V. Marejeleo HAMNA

Mmiliki Anayewajibika:	Fedha – Usimamizi wa Mapato	Mawasiliano:	Kimberly Mender
Imeidhinishwa Na:	Ofisi ya Msaada wa Sera; Ofisi ya Msaada wa Sera – Sera za Kikundi Pekee; Mender, Kimberly; Muhlen, John; Perras, Joseph; Wood, Gary	Toleo Namba:	6
Tarehe ya Sasa ya Kuidhinishwa:	10/08/2025	Kitambulisho cha Hati ya Zamani:	
Tarehe ya Sera Kuanza Kutumika:	10/08/2025		
Sera na Taratibu Husika:			
Vifaa vya Kazi Vinavyohusiana:			